

## HAKI NITAKUWA BWANA

1. Jina la Mola nanzie, kukuomba Maulana,  
Kwa jinalo niishie, nikimaliza kunena,  
Mola wangu nijalie, watu waniite bwana,  
Haki nitakuwa bwana, roho ya baba kifata.
2. Rabana nihurumie, watu waniite bwana,  
Wasisje wanitanie, matusi kunitukana,  
Rajabu nimfatie, roho yake sana sana,  
Haki nitakuwa bwana, roho ya baba kifata.
3. Kaumu inisifie, kuwa Hamidu mwanana,  
Wengi niwasaidie, kama wana shida sana,  
Pia niwatimizie, wenye shida za maana,  
Haki nitakuwa bwana, roho ya baba kifata.
4. Na tena anijalie, nikusabihi Rabana,  
Sala nisiichie, nikajitia ubwana,  
Na baba umjalie, aache sala kukana,  
Haki nitakuwa bwana, roho ya baba kifata
5. Na dini niitambue, mithili ya Rajabana,  
Na sheria nizijue, kama yeye muungwana,  
Kwa hizo nijivunie, dini kuijua sana,  
Haki nitakuwa bwana, roho ya baba kifata.
6. Neema unijalie, Mola wangu Maulana,  
Fani ya Rajabu iwe, baba yangu muadhana,  
Huo ubaya utoe, iwe ya Rajabu fana,  
Haki nitakuwa bwana, roho ya baba kifata.
7. Ungole uniondoe, kama Rajabu Kamwana,  
Ukweli unijazie, ukweli wa sana sana,  
Kaumu inisifie, kwa hayo wanite bwana,  
Haki nitakuwa bwana, roho ya baba kifata.
8. Kujitweza nisijue, kama ya Rajabu fana,  
Na mlenda nijilie, bila ya kuutukana,  
Na chini nijilalie, endapo ni mubahana,  
Haki nitakuwa bwana, roho ya baba kifata.
9. Ndugu niwasaidie, kama Kisamba mwanana,  
Na wote niwangalie, kama wanasadiana,  
Wavivu niwaondoe, athira yao vijana,  
Haki nitakuwa bwana, roho ya baba kifata.
10. Hata kesho nijifie, wanitie jenezana,  
Na kisha wakumbukie, niliyotenda kijana,  
Na hatimaye walie, kunikumbuka kijana,  
Haki nitakuwa bwana, roho ya baba kifata.
11. Hatima niifikie, nisiombe mengi sana,  
Na mwishoni niishie, kwa jina lako Rabana,  
Muhammadi zimwendee, rehemazo Subhana,  
Haki nitakuwa bwana, roho ya baba kifata.
12. Dua utakabalie, Amina Mola Amina,  
Dua usiziachie, dua zangu Maulana,  
Mola wangu nijalie, watu, mtu kuniona,  
Haki nitakuwa bwana, roho ya baba kifata.

**HRST/hrst**  
**MBEYA**  
**09/11/1967**